JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

# MAJIBU YA MASWALI YALIYOULIZWA NA WAHESHIMIWA WABUNGE

## WA KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI PAMOJA NA MAONI NA USHAURI

TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA

(TACAIDS)

## UTANGULIZI

Mnamo tarehe 11 Aprili, 2008 Kamati ya Bunge ya UKIMWI ilikutana na Uongozi wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania . Baada ya uwasilishaji wa mada mbalimbali kutoka kwa Mwenyekiti Mtendaji na wakurugenzi wa Tume, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kutoa maoni na kuuliza maswali ili kupata ufafanuzi katika baadhi ya mambo muhimu yanayohusu uratibu na utekelezaji wa mapambano dhidi ya UKIMWI nchini.

Ufuatao ni muhtasari wa majibu ya uongozi wa Tume juu ya maswali na hoja mbalimabli za waheshimiwa wabunge. Maswali na hoja zimechapwa katika wino mzito na majina ya waheshimiwa wabunge waliouliza yako kwenye mabano. Majibu yanafuata chini ya maswali/hoja kwa wino wa kawaida.

**Mh.Paul Peter Kimiti, (MB), Sumbawanga Mjini:**

1. **Kuanza kuweka sheria kabla ya kurekebisha sera haikuwa busara hata kama ni kwa uharaka uliokuwapo**

*Ni kweli kuwa Sheria ilitungwa kabla ya Sera kurekebishwa; hii inatokana na ukubwa wa tatizo hili ndiyo maana ilifanyika hivyo . Ili kurekebisha kasoro hii, Serikali sasa kwa upya imepanga kufanya mapitio ya Sera ya UKIMWI Tanzania na pia na Sheria iliyounda Tume ya Kudhibiti UKIMWI ili ziboreshwe na kuhakikisha kuwa vinawiana*

**Mh. Paul Peter Kimiti, (MB), Sumbawanga Mjini:**

2. **Takwimu zikitumiwa vibaya kunakuwa na shida, nashukuru sasa mnatambua umuhimu wa Takwimu**

*Ni kweli kuwa kama takwimu zitatumika vibaya zinaweza kutoa taswira na maana tofauti. Ili kusahihisha hili, Tume inaendelea kuelimisha wadau wa ngazi zote namna ya kukusanya , kuchambua kutafsiri na matumizi ya takwimu za UKIMWI*

**Mh.Paul Peter Kimiti, (MB), Sumbawanga Mjini:**

3. **Rukwa kuna Vikundi vitatu kwa nini?**

*Asasi za kiraia zinaanzishwa kwa hiari. Hivyo uchache wa vikundi ama Mkoa fulani unaweza kuwa unatokana na mwamko ulioko kwenye Mkoa husika. Kwa kupitia TASAF, vikundi vya Jamii kutoka Mikoa yote (hata ile Mikoa yenye asasi za jamii chache) itaweza kusaidiwa kupunguza kasi za maambukizo mapya na kumudu makali ya waliyoathirika.*

**Mh.Paul Peter Kimiti, (MB), Sumbawanga Mjini:**

**4. Unyanyapaa ulikuwepo kuanzia zamani, ni vizuri kuwahusisha jamii na viongozi kama wabunge na viongozi wa dini. TACAIDS iwawezeshe wanakamati wa bunge mara kwa mara ili itambue hali halisi ili na wao wasaidie serikali namna bora ya kuangalia hasa maeneo yaliyoathirika zaidi**

*Tume itajitahidi kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge hususani walio kwenye Kamati ya Kudumu ya UKIMWI kutokana na uwezo uliopo. Rai yetu kwenu ninyi Waheshimiwa ni kuomba muendelee kushiriki hasa kwenye majimbo yenu kupitia Kamati Shirikishi za Kupambana na UKIMWI (CMACs) ili kufanikisha mapambano haya ambayo yanahitaji mchango wa kila Mtanzania*

**Mh.Elietta Nandumpe Switi, (MB), Viti Maalum:**

**5. Jitihada za chanjo ya UKIMWI zimefika wapi?**

*Tangu tupate matukio ya ugonjwa huu nchini (1983) na duniani, nchi nyingi zimeweka jitihada katika suala la utafiti. Kwa nchi yetu utafiti huu unafanywa katika Hospitali ya Rufaa ya Mbeya ambapo Serikali inashirikiana na Serikali ya Marekani na Serikali ya Ujerumani. Aidha, utafiti mwingine unafanywa na Chuo Kikuu cha Sayansi ya Jamii Muhimbili na Hospitali ya KCMC. Matokeo bado hayajatoa matunda kwetu na duniani kwa ujumla kutokana na ugumu wa maumbile ya virusi kuwa vinabadilika-badilika. Kila matokeo yatapopatikana taarifa itatumwa kwa kamati hii. Aidha Tume ya kudhibiti UKIMWI inashauri kuwa mtakapopanga sehemu za kutembelea, muwasiliane na Sekta ya Afya ili mpange kutembelea sehemu ya utafiti huu, Hospitali ya Mbeya*

**(Mh.Elietta Nandumpe Switi, (MB), Viti Maalum)**

**6. Nini Kifanyike ili TAKWIMU ziwe sahihi?**

*Tume inafanya jitihada kuhakikisha inaandaa mifumo na miundo ya ukusanyaji na tafsiri ya takwimu inafanyika kwa misingi ya kuzingatia ubora wake kwa kutumia Principle ya THREE IN ONE : Kwa maana ya kuwa na Taasisi moja ya uratibu , Mkakati mmoja na Mfumo mmoja wa takwimu katika nchi. Vile vile jitihada ya kukusanya takwimu kutoka kila sekta na kutoka jamii inaboreshwa. Tunategemea matokeo ya utafiti wa UKIMWI na malaria uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya TAKWIMU kwa kushirikiana na TACAIDS na Wizara ya Afya kuwa tayari ifikapo mwezi wa Juni 2008. Utafiti huu utaonesha kasi na ukubwa wa maambukizo kwa kila Mkoa wa Tanzania bara na Zanzibar, ufahamu wa watu kuhusu UKIMWI, vihatarishi na huduma zilizopo*

**Mh.Elietta Nandumpe Switi, (MB), Viti Maalum:**

**7.Tufanye nini ili wananchi watusikie na kubadilisha tabia hatarishi?**

*Inabidi Viongozi wetu wa kisiasa, Dini, Jamii na viongozi wa Mila kuunganisha nguvu katika mapambano dhidi ya UKIMWI kwani katika janga hili nguvu ya pamoja inahitajika. Ni budi kila mmoja katika nafasi yake ahamasishe eneo lake kwa nguvu zake zote, hasa tukielewa kuwa kubadili tabia huwa kunatokea pole-pole.*

**Mh.Elietta Nandumpe Switi, (MB), Viti Maalum:**

**8. Wakala wa TACAIDS (Regional Facilitating Agencies – RFA) wanaondoka mikoani, TACAIDS ina mpango gani kwa sasa?**

*Ili kuendeleza shughuli zilizokuwa zinafanywa na RFA, Tume ya Kudhibiti UKIMWI imeingia mkataba na TASAF ili vikundi vya kijamii viweze kuendelea kupata msaada wa kifedha na kiufundi utaowawezesha kujikinga na kupunguza kasi za maambukizo na athari ya maambukizo.*

**Mh.Elietta Nandumpe Switi, (MB), Viti Maalum:**

**9. Nashauri TACAIDS ianzishe miradi midogo-midogo badala ya kutoa pesa taslimu?**

*Hili ni angalizo zuri, tutalizingatia*

**Mh.Omar Shaaban Kwaangw' (MB) Babati Mjini:**

**10. Changamoto kwenye mada ya fedha na rasilimali za UKIMWI TACAIDS iwe inatusaidia kupata mtiririko wa taarifa za pesa ili kamati na Wabunge wazifahamu**

*Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wahisani mbalimbali ili fedha zipitie kwenye mifumo ambayo Serikali itaweza kupata taarifa na kuelezea matumizi ya fedha hizo. Taarifa za fedha zilizo kwenye MTEF za Wizara, Idara na Taasiss zake zinapitia Bunge, kwa hiyo ziko wazi zinafahamika. Orodha ya taasisi za kiraia zilizopata fedha kupitia Wakala kwa mwaka 2007 zitawasilishwa kwa Kamati ya UKIMWI ya Bunge kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu.*

**Mh.Omar Shaaban Kwaangw' (MB) Babati Mjini:**

**11. Wingi wa NGO una uhusiano na kiwango cha maambukizi? maana tofauti ni kubwa sana. Taarifa za rasilimali za UKIMWI ziendazo kwenye asasi zisizo za Serikali ziwafikie District Consultative Committees**

*Wingi wa Asasi za Kiraia mara nyingi hutokana na mwamko wa wananchi na wadau katika sehemu husika, na sio wakati wote kutokana na ukubwa wa maambukizo. Asasi hizi husaidia kufikisha huduma na elimu kwa*

*jamii pana zaidi. Halmashauri zimekuwa zikifanya kazi ya kutambua na kuratibu kazi za baadhi ya asasi. Kunahitajika bidii zaidi ya kufanikisha uratibu wa Halmashauri.*

**Mh.Omar Shaaban Kwaangw' (MB) Babati Mjini:**

**12. Tatizo la UKIMWI ni kubwa sana mkoa wa Manyara licha ya mkoa kuwa mchanga**

*Ni kweli kuwa tatizo la UKIMWI bado ni kubwa katika nchi na Mkoa wa Manyara ukiwemo. Tunafikiri kabla ya mwisho wa mwaka tutapata matokeo ya utafiti wa viashiria unaofanywa na utatoa ukubwa wa tatizo hili kwa kila Mkoa. Tuta andaa mikakati ya kushughulikia baada ya takwimu hizi kuwa tayari ili kuwa na mikakati ya kudhibiti maambukizi mapya kwa Jamii ya wafugaji wa Mkoa wa Manyara, Arusha pamoja na mikoa mingine yenye wafugaji*

**Mh.Dr. Zainab Amir Gama (MB) Kibaha Mjini:**

**13. Shukrani kwa TACAIDS kwa kutupa uelewa; pesa zimeletwa japo tunajichanganya juhudi nyingi zimefanyika lakini je research zimefanyika? Kwa nini UKIMWI unaendelea pamoja na juhudi zote?**

*Tume inachukua hili kama changa moto kuwa na mkakati wa makusudi kutoa takwimu zinazohusu fedha kwa Jamii wakiwemo Waheshimiwa Wabunge.*

*Ni kweli kuwa UKIMWI bado ni tatizo pamoja na juhudi zinazofanyika na zilizofanyika. Inaonekana kuwa kuna viashiria vinavyochochea UKIMWI nchini kwa makundi yote kama vile mila, desturi. Hayo yalikuwa hayajaangaliwa kwa makini. Pia kuna makundi ambayo yanahitaji nguvu za ziada ili kusimamisha maambukizi Makundi haya yakiwa ni pamoja watu wanaouza/kununua ngono (commercial sex workers and their partners); watu ambao kazi zao zinawafanya waishi mbali na familia zao (madereva wanaoenda nje ya nchi, wanaojenga barabara, wasafiri wa mara kwa mara, wavuvi na wanunuzi wa samaki n.k.) Serikali na wadau inaendelea kuandaa mkakati na vipaumbele vya utafiti ambavyo vitatatua matatizo haya na mapungufu yanayojitokeza*

**Mh.Dr. Zainab Amir Gama (MB) Kibaha Mjini:**

**14. Uhusiano wa UKIMWI na uchumi haujazungumziwa**

*UKIMWI kama ugonjwa una madhara katika uchumi wa nchi kwa vile unaua nguvu kazi, unafanya watu wasiende kazini wakiwa wagonjwa, unatumia rasmali kubwa sana kutibu na kuzuia na pia umri wa kuishi wa watu nchini unapungua. Kwa misingi hii kuna mahusiano makubwa kati ya UKIMWI na uchumi wa nchi.*

**Mh.Dr. Zainab Amir Gama (MB) Kibaha Mjini:**

**15. Umri unaochochea ngono (adolscents) umefanyiwa afua gani ya kuudhibiti?**

*Asasi nyingi za Serikali, zisizo za serikali na asasi za dini zimekuwa zinaendesha elimu hasa ya kinga kwa vijana waliyo shuleni na walio nje ya shule. Utafiti unaonesha kuna mafanikio, ijapokuwa ni dhahiri kuwa kazi ya kubadili tabia inahitaji kuendelea na afua zinazofaa. Inadhaniwa kuwa Kampeni ya Serikali ya kueneza elimu, kuongeza na kuboresha shule inamchango mkubwa kwenye kuzuia UKIMWI kwa vile sekta ya elimu ina masomo maalumu ya UKIMWI.*

**Mh.Dr. Zainab Amir Gama (MB) Kibaha Mjini:**

**16. Mnafanyaje kutambua thamani ya pesa (value for money) na afua zilizofanyika?**

*Wakaguzi wa hesabu wa taifa na hata mkaguzi wa ndani wa Tume wametengeneza vigezo vya kupima thamani ya pesa wakati wanapoenda kufanya ukaguzi wa hesabu kwa watekelezaji wa shughuli za UKIMWI za Wizara na Idara za Serikali, Halmashauri na Asasi zisizo za Serikali.*

- *Thamani ya fedha kuhusiana na huduma itolewayo huhakikiwa kuanzia wakati wa maombi ambapo michanganuo yote hupitiwa na wataalamu ili kuona miongozo, sera na mikakati ya Taifa imefuatwa;*
- *Wakati na baada ya utekelezaji, shughuli zote hufuatiliwa kuhakikisha utekelezaji unaenda sawa kadri ya makubaliano*

*Tathmini ya kitaalamu pia hufanyika ili kupima matokeo ya afua mbalimbali iwapo zinasaidia kufikia lengo/ malengo*

**Mh.Dr. Zainab Amir Gama (MB) Kibaha Mjini**

**17. Pesa nyingi zinazotolewa na mradi wa Marekani hazifikii walengwa kama wao wanang'ang'ania ziende kwenye NGO zifanye peke yake. Tutumie CMACs kufanya tathmini ya pesa inayotumika**

*Mkakati uliopo sasa ni wa kuboresha kazi za CMACs, ili ziweze kusaidia kuboresha matumizi ya fedha za UKIMWI zikiwemo na zinazotoka Serikali ya Marekani.*

*Hatuna ushahidi wa kutosha kuwa fedha nyingi za Wamarekani haziwafikii walengwa lakini kwa vile fedha ya Wamarekani haijulikani kwenye vitabu vya Serikali kutokana na ukweli kwamba zinaenda moja kwa moja kwenye asasi za kiraia, Serikali imeanza kuwabana Wamarekani kwa kuwataka wawe na utaratibu unaojulikana ili Serikali iweze kujua na kuingiza fedha hizo kwenye vitabu vyake*

**Mh.Dr. Zainab Amir Gama (MB) Kibaha Mjini:**

**18. CMACs hamna wanachofanya huko kwenye jamii**

*Ni wazo, lakini inastahili jibu. Kusema kuwa CMACs hakuna inachofanya kwenye jamii itakuwa ni kuangalia upande mmoja tu wa shilingi. Kwanza ikumbukwe kuwa CMACs ni mfumo mpya ulioanzishwa na TAMISEMI kwa ajili ya kuratibu masuala ya UKIMWI kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. CMACs ni moja ya Kamati za Kudumu kwenye Halmashauri ambapo pia Wah. Wabunge ni wajumbe. Waheshimiwa Wabunge wana uwezo mkubwa wa kuzifanya CMACs zifanye kazi pale ambapo wanaona hazifanyi hivyo. Sauti zenu ni kubwa sana kuweza kuzifanya CMACs zitekeleze majukumu waliyopangiwa.*

**Mh.Dr. Zainab Amir Gama (MB) Kibaha Mjini:**

**19. RFA hawajui tamaduni zetu, mmechaguana kwa kujuana kwenu, nimejipendekeza kwao bila mafanikio, nadhani tutafute njia zingine - RFA wameshindikana**

*Wengi wa RFAs ni asasi za kiraia zilizopo nchini na hivyo ni za Watanzania kwa hiyo tunategemea kuwa wanajua tamaduni zetu. RFAs walichaguliwa kwa kufauata mchakato uliowekwa na Serikali. Asasi nyingi (75) zilikuwa zimeomba na baada ya mchakato kupitia Central Tender Board zilichaguliwa asasi 11 kuwa RFAs. Hivyo hawakuchaguliwa kutokana na kujuana. Hata hivyo mikataba ya RFAs inakwisha na TACAIDS imeandaa utaratibu mpya wa kuwa na makubaliano na TASAF. Hivi sasa RFAs 7 wamemaliza mikataba yao na TASAF wamechukua nafasi hizo. TASAF watashughulikia vikundi vya kijamii.*

**Mh.Dr. Zainab Amir Gama (MB) Kibaha Mjini:**

**20. Zoezi la kupima ni zoezi zuri sana lakini hakuna ushauri nasaha unaofanyika.**

*Utaratibu uliopo ni kuwa mtu kabla hajapima ni lazima apewe ushauri nasaha na hili zoezi liliendeshwa katika mfumo huu. Kama kuna mapungufu basi tutashirikiana na Wizara ya Afya kurekebisha*

**Mh.Dr. Zainab Amir Gama (MB) Kibaha Mjini:**

**21. Kumbumumbu zetu za kuhusu UKIMWI ulivyoanza nchini zinaonesha kuwa mtu wa kwanza mwenye dalili za UKIMWI alijitokeza 1979 Hospitali ya KCMC na sio 1983 kama inavyozungimziwa**

*Ni kweli kuwa mgonjwa wa kwanza inawezakana kuwa alipatikana kabla ya mwaka 1983 aliyeonekana KCMC. Lakini kisanyasi tunatumia Takwimu ambazo zilithibitika kitaifa na kimataifa. Ijapokuwa sio rahisi kutekeleza, ushauri umepokelewa kuwa wataalamu tuendelee kufuatilia ili ipatikane historia hii kwa kumbukumbu*

**Mh.Cynthia Hilda Ngoye (MB) Viti Malum:**

**22. Uratibu wa mikoa na wilaya tunazotoka kuna afua nyingi sana za kudhibiti UKIMWI ila zote ni za aina gani?**

*Afua nyingi zinazotekelezwa na wadau zimejikita kwenye kutoa matunzo na misaada na kuelimisha jamii. Ni afua chache tu ambazo zinalenga kwenye kinga kamili ya maambukizi*

**Mh.Cynthia Hilda Ngoye (MB) Viti Malum**

**23. Asasi hizo zinaonekana kuto kuwa na mgawanyo wa majukumu kulingana na kipaumbele cha Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa awamu ya pili. Kuna haja ya kuzifahamu asasi hizi na kujua wanachokifanya na mafanikio yanayopatikana**

*Kwenye Halmashauri mwongozo wa namna ya kupanga mipango ya UKIMWI hutolewa (Minimum Package). Mwongozo huo unaonesha maeneo dhamiriwa kulingana na mkakakti. Hata hivyo kwenye Asasi za Kiraia ni vigumu kulazimisha ufuataji wa Package hiyo kwani mara nyingi asasi za kiraia hupanga kutekeleza kile wanachokimudu zaidi kiutaalamu na kiufundi*

*Halmashauri zina nafasi nzuri kupanga na asasi za jamii juu ya maeneo yanayostahili kupewa kipaumbele.*

**Mhe. Dr. Binilith Satano Mahenge (MB), Makete**

**25. TACAIDS isaidie kuahirisha tatizo la UKIMWI Makete na jinsi ya kusaidia**

*Wazo la Mhe. Mbunge ni zuri na ni mategemeo ya kila mtu na wanaharakati. Tunaomba tusaidiane pia na Waheshimiwa Wabunge katika kuelimisha Jamii iweze kujikinga na UKIMWI*

**Mhe. Dr. Binilith Satano Mahenge (MB), Makete**

**26. Uhusiano kati ya umaskini na UKIMWI**

*Jibu lake ni sawa ambalo limejibiwa katika jibu la msingi kwa Mhe. Dr Gama (suala namba 14)*

**Mhe. Dr. Binilith Satano Mahenge (MB), Makete**

**27. Pesa ya serikali zinaenda sehemu tatu, hamna component ya kujenga Uchumi wa eneo husika.**

*The issue is not clear to me*

**Mhe. Dr. Binilith Satano Mahenge (MB), Makete**

**28. Njia pekee ya Kuonda tatizo ni kuhakikisha huduma ya kuelimisha kuhusu kinga ya UKIMWI ifikie mpaka kwenye ngazi ya kaya**

*Ni wazo zuri ambalo pia limejitokeza kwenye Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI. Kufikia ngazi ya kijiji na kaya kupewa kipaumbele sana katika mwitikio wa UKIMWI.*

**Mhe. Dr. Binilith Satano Mahenge (MB), Makete:**

**29. Tuzungumze na wanaotoa misaada ya pesa ili tuyafahamu maeneo yaliyofanikiwa na ni kwa kiasi gani yamefanikiwa isije kuwa misaada hiyo inalenga kutoa ajira kwa wananchi wao tu.**

*Kuhusu uwazi wa rasmali za UKIMWI zinazoletwa na wahisani wetu ni tatizo sugu kwa kuwa baadhi hawako wazi licha ya kuwa, Paris na Rome Decleration linaelekeza jumuiya ya kimataifa inayotoa misaada kuwa wazi bado hatujafanikiwa vizuri.Tutaendelea kujadiliana ili kuboresha hili. Majadiliano yanayoendelea sasa baina ya Serikali na wadau wa Maendeleo yanaleta matumaini ya tatizo hili kupungua kwa kiasi kikubwa.*

**Mhe. Dr. Binilith Satano Mahenge (MB), Makete:**

**30. Tafiti iwepo ili tujue mbali na maeneo ainishwa ni vipi tunaweza kuhangaika kuondoa ugonjwa wa UKIMWI. Kuna wasiwasi kuwa UKIMWI umetokana na mkakati wa kuangamiza Afrika.**

*Pamoja na kuwa ni vigumu kusema kuwa tutaondoa UKIMWI kwa misingi namna unavyoenea na kuwa ni ugonjwa unaohitaji Jamii kubadili tabia zao; Serikali na wadau wa asasi zisizo za serikali zinaendelea kuelimisha Umma ili jamii ijikinge na Ugonjwa huu. Hili linahitaji nguvu ya kila mmoja wetu pamoja na nyinyi Waheshimiwa Wabunge.*

**Mhe. Fuya Godwin Kimbita (MB), Hai:**

**31. Tatizo la kupata taarifa kutoka kwa RFA, Waheshimiwa Wabunge wapewe taarifa ya kinachoendeklea- RFA/ Wilaya na Halamashauri na mipango baada ya RFA kuondoka**

**Vikao vya CMAC mara nyingi vinafanyika wakati Waheshimiwa Wabunge hawapo**

*Taarifa za RFAs zipo, TACAIDS inaahidi kutuma nakala Ofisi za Bunge, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu.*

*Kuhusu mipango baada ya RFAs kuondoka Tume imeingia mkataba wa mwaka mmoja na TASAF ili kukamilisha awamu ya Mradi wa Benki ya Dunia. TASAF watashughulikia vikundi vya jamii.*

*Ushiriki wa Waheshimiwa Wabunge kwenye kamati za CMACs ni muhimu sana. Ushiriki wao utatoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge kuchangia, kuboresha na kushiriki kwenye afua za kupunguza mapambano na kusaidia wale waliopata maambukizo.*

*TACAIDS inashauri suala hili lijadiliwe kwenye kila jimbo ili lipate ufumbuzi wa kudumu*

**Mhe. Fuya Godwin Kimbita (MB), Hai:**

**32. Vigezo vya kupeleka pesa Mkoani ni vipi?**

*Serikali inatumia vigezo vifuatavyo kupeleka fedha mikoani:*

1. *Idadi ya watu kwa kila Halmashauri – kutokana na Census*
2. *Kiwango cha umaskini*
3. *Ukubwa wa eneo katika kutoa huduma za Afya*
4. *Kiwango cha maambukizi ya UKIMWI (kwa kutumia takwimu za Mkoa kama zinavyooneshwa na utafiti wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu ).*

**Mhe. Fuya Godwin Kimbita (MB), Hai:**

**33. Pamoja na pesa taslimu mipango ya kuwapa yatima virutubisho na vyakula iimarishwe zaidi kuliko kuwapa pesa**

*Utafiti uliofanyika Vyuo Vikuuu vya Muhimbili kwa kushirikiana na Harvard umeonesha ni vurutubisho vipi vilivyomuhimu kwa watu wazima na watoto wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Sekta ya Afya, ikijumlisha Shirika la Chakula na Lishe na asasi za kiraia zinatoa huduma kwa yatima wanaostahili na kuhitaji msaada*

**Mh.Chacha Zakayo Wangwe (MB) Tarime;**

**34. Tangu 1983, hadi sasa kuna kubabaika sana kuhusu chanzo cha UKIMWI. Wengine wanamawazo kuwa UKIMWI ulitengenezwa kwenye chupa kwenye mwaka 1953, Ukweli ni upi? Sera kamili ya kushughulikia UKIMWI iandaliwe, takwimu zinaonesha UKIMWI unaongezeka.**

*Kuna maoni tofauti ya kuhusu chanzo cha ugonjwa wa UKIMWI na ni lini ulianza na wapi. Serikali imeona ni busara kujikita zaidi kwnye kupunguza kasi za maambukizo na kuboresha hali na afya ya wale ambao wana maambukizo au kuathirika kwa namna nyengine*

*Serikali itapitia sera ya UKIMWI ya 2001 ambapo tutaainisha sera ya kushughulikia suala hili kwa misingi ya Mkakati mpya wa 2008/2012*

**Mh.Chacha Zakayo Wangwe (MB) Tarime;**

**35. Tuwatazame kwa makini wa Marekani kwa kuwa wao ni “master of confusion creators”**

*Serikali imekuwa inafanya kazi kwa ukaribu. Msaada wa Marekani umeiwezesha nchi kuongeza nguvu zake kununua dawa za kupunguza makali ya maambukizi, kujenga maabara na kununua vitendea kazi vyake; kutoa fedha kwa asasi zisiso za serikali zinazo toa huduma ya matibabu kwa watoto, kwa vijana, kuhudumia yatima n.k*

**Mh.Chacha Zakayo Wangwe (MB) Tarime**

**36. UKIMWI umetengenezwa kumaliza watu Fulani duniani hivyo tutazame upya vyanzo vya ugonjwa huu.**

*Hakuna uthibitisho wa dhana za chanzo cha UKIMWI; linalotiliwa mkazo wa Serikali ni kuhakikisha kuwa maambukizo mapya yana pungua na pia athari kwa wale ambao tayari wameambukizwa zinapungua na wanapata matibabu stahili*

**Mh.Chacha Zakayo Wangwe (MB) Tarime**

**37. Marekani hawawezi kuwa na nia ya dhati ya kumaliza UKIMWI tuwatazame**

*Serikali ya Marekani ni mmoja wa wachangiaji wakubwa wa udhibiti wa UKIMWI nchini. Serikali inatambua mchango wao hasa kwa sekta ya Afya, ikiwemo ununuzi wa dawa za kupunguza makali ya maambukizi, kusaidia ubora na wingi wa maabara na huduma zake, kutoa mafunzo kwa wataalamu, kutoa huduma za UKIMWI jeshini, utafiti n.k. Serikali inaendelea na majadiliano ili fedha zinazoingia nchini zifahamike kwa uwazi zaidi.*

**Mh.Chacha Zakayo Wangwe (MB) Tarime:**

**38. Watu wanaweza kuacha Ngono wakipewa elimu fasaha**

*Ni kweli kabisa watu wataacha au watafanya ngono salama pale tu watakapopewa taarifa na elimu sahihi ya kubadili tabia za mahusiano ya ngono. Ni kweli pia kuwa kwa vile ubadili wa tabia sio jambo linalotokea kwa haraka, elimu inahitaji iendelee, ilenge makundi mbalimbali, iwe inajulisha masuala ya vihatarishi, jinsia na maswala ya mila na desturi hatarishi*

**Mh.Chacha Zakayo Wangwe (MB) Tarime:**

**39. Siamini katika matumizi ya Condom kwa kuwa inamaanisha hatutabadilika**

*Kitendo cha kutumia kondom tayari ni hatua moja wapo ya kubadili tabia maana watumiaji wanafanya ngono salama. Kwa wale ambao hawataki au hawawezi kutumia kondom, inabidi aidha wasifanye ngono, au wapime afya yao kama inavyoshauriwa, endapo hawana maambukizo, na waendelee na mpenzi mmoja tu ambae nae hana maambukizo*

**Mh.Chacha Zakayo Wangwe (MB) Tarime:**

**40. Siamini kama Kondom inazuia UKIMWI kwa asilimia 100.**

*Imethibitishwa kitaalamu kuwa kondom ikitumika ipasavyo, kila mara mtu anapofanya ngono inazuia UKIMWI kwa asilimia 100.*

**Mh.Chacha Zakayo Wangwe (MB) Tarime:**

**41. Ili tuweze kusihi watu wapime - waliotharika watambulike bayana.**

*Kampeni ya kupima ni nzuri sana na ni vyema watu wote wakaendeleza tabia ya kupima ili kujua afya zao lakini sheria ya nchi yetu imeweka wazi kuwa kujitangaza ni hiari ya mtu - asilazimishwe.*

**Mh.Kidawa Hamid Saleh (MB) Viti Maalum:**

**42. Watoto wanaoishi katika mazingira magumu ni matokeo ya UKIMWI. Je elimu kwa watoto hawa inaandaliwaje?**

*Watoto waishio katika mazingira magumu ni kweli wameongezeka zaidi kwa sababu ya UKIMWI. Wizara ya Elimu inatoa elimu ya UKIMWI kupitia mitala ya shule.*

*Mashirika mengi yanatoa huduma kwa watoto na vijana yatima. Huduma hii ni pamoja na elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya juu. Kuna haja ya kuboresha mfumo wa kupata takwimu sahihi zinazoonesha idadi kamili ya wanaopata msaada kwa kulinganisha na wale ambao wanahitaji msaada lakini hawapati. Hii itawezesha wadau kulenga huduma kwa wale ambao wanastahili lakini hawapati.*

**Mh.Kidawa Hamid Saleh (MB) Viti Maalum:**

**43. Utafiti wa dawa za mitishamba ambazo inasemekana zinatengeneza hata dawa za kisasa unapewaje kipaumbele**

*Wizara ya Afya ina kitengo cha dawa za asili na kitengo hichi kinafanya kazi kwa karibu na waganga wa jadi.*

*Kuna baadhi ya dawa mbazo zimeonekana kuwa na muelekeo wa kupunguza makali ya magonjwa yanayojitokeza na UKIMWI. Hata hivyo, bado hakuna dawa ya kuponyesha UKIMWI*

**Mh.Kidawa Hamid Saleh (MB) Viti Maalum:**

**44. Mkazo katika watu wanaooana kupima umewekewa mikakati gani?**

*Kupima **kwa hiari** ni jambo zuri lenye faida nyingi*

**Mh. Maria Ibeshi Hewa (MB) Viti Maalum:**

**45. NGO za mifukoni ni nyingi sana katika jamii zetu je TACAIDS inajihusishaje kutambua NGO za ukweli na za mifukoni?**

*Utambuzi wa Asasi za kiraia ulifanyika kwa kutumia zana iitwayo CSO Mapping and Assessment. Zana hii ndani ya mchakato wake huwahusisha jamii zinazohudumiwa na asasi hiyo watoe maoni yao kuhusu hiyo asasi. Endapo kuna NGOs za mfukoni, kwa kutumia zana hii ukweli unaweza kuonekana na hivyo kutokidhi vigezo vya ufadhili.*

**Mh. Kabuzi:**

**46. Makundi maalum kama vile wavuvi na wachimbaji madini wanaojitokeza katika kupanmbana na UKIMWI wanasaidiwaje?**

*Misaada kwa ajili ya makundi maalum pia ilitolewa na RFAs. Kwa kuwa sasa baadhi ya RFAs wamemaliza mikataba yao, utaratibu mpya unaangaliwa namna ya kuendelea kuyashughulikia makundi hayo.*

**47. Mwenyekiti mtendaji akayashughulikie maswali haya kisha atafute siku nyingine kwa ajili ya kuyajibu (Mh. Dr. Luka Jelas Siyame, (MB), Mbozi Magharibi)**

*Maswali yote yamejibiwa na wataalamu wa TACAIDS na kukabidhiwa Ofisi ya Waziri Mkuu ili yafikishwe kwenye Kamati ya UKIMWI ya Bunge. Endapo itahitajika kuwa na mikutano mingine, Tume itakuwa tayari kukutana na kamati.*

**48. Kuwe na Vikao vya mara kwa mara.(Mh. Dr. Luka Jelas Siyame, (MB), Mbozi Magharibi)**

*Pendekezo limepokelewa; tutashauriana na Ofisi ya Waziri Mkuu ili kila inapohitajika kuwe na uwezo wa Kamati ya UKIMWI ya Bunge iweze kukutana na wadau mbali mbali kutegemea na kuwepo kwa rasilimali. Tunashauri Kamati ya UKIMWI ya Bunge itayarishe bajeti ya mikutano ya UKIMWI inayoiona ina umuhimu na kuiitengea fedha.*

Barabara ya Sokoine na Morogoro
Jengo la Old Boma
S.L.P. 76987 Dar es Salaam

Simu: +255 22 2122651, 2125127
Fax: +255 22 2122427
Tovuti: www.tacaids.go.tz